


## Je, Kuna Viti Vingapi vya Enzi?

Danieli 7:9 inasema kuna viti vya enzi mbinguni. Hapo wapo watu wanaotumia sehemu hiyo ya maandiko kuhitimisha kuwa Mungu anaviti vya enzi vitatu, yani kiti cha Mungu Baba, Mungu Mwana na Mungu Roho Mtakatifu. Sasa Je, Mungu ana viti vingapi anavyovikalia mbinguni?

**Majibu:**

Ukweli ni kwamba, Mungu ni mmoja na kiti cha enzi cha Mungu ni kimoja, japo mbinguni kuna viti vya enzi vingi. Tazama ushahidi huu wa kimaandiko:

> *Nikatazama hata viti vya enzi vikawekwa, na mmoja aliye mzee wa siku ameketi; mavazi yake yalikuwa meupe kama theluji, na nywele za kichwa chake kama sufu safi; kiti chake cha enzi kilikuwa miali ya moto, na gurudumu zake moto uwakao.*
> *~ Danieli 7:9*

Kwa mujibu wa Danieli, kuna viti vingi vya enzi mbinguni, lakini Mungu anakiti chake ambacho kinaelezwa kuwa tofauti na viti vingine vya enzi. Zipo aya nyingine zinafafanua kuwa hivi viti vingine vya enzi ni vipi, tazama hapa:

> *mpate kula na kunywa mezani pangu katika ufalme wangu; na kuketi katika viti vya enzi, huku mkiwahukumu kabila kumi na mbili za Israeli.*
> *~ Luka 22:30*

> *Na wale wazee ishirini na wanne waketio mbele za Mungu katika viti vya enzi vyao wakaanguka kifulifuli, wakamsujudia Mungu*
> *~ Ufunuo 11:16*

Kwa aya hizo, kuna viti vya enzi vya watu watakao-okolewa, kuna viti vya enzi vya wale wazee ishirini na nne na kisha kuna kiti cha enzi cha Mungu. Mungu hana viti vya enzi, ana kiti cha enzi. Ushahidi wa maandiko.

### Ushahidi wa Maandiko wa Kiti Kimoja cha Enzi cha Mungu

> *Nilikiona kiti cha enzi, na juu yake aliketi Baba na Mwana. Niliutazama uso wa Yesu na nikastaajabu jinsi alivyo mzuri. Nafsi ya Baba sikuweza kuiona, kwa maana wingu la utukufu lilimfunika. Nilimuuliza Yesu kama Baba Yake ana umbo kama Yeye mwenyewe. Alisema analo, lakini sikuweza kuliona, maana alisema, "Kama utauona utukufu wa nafsi yake, utakoma kuishi." ~ Early Writtings 54.2*

Hapo kiti cha enzi cha Mungu kinaonekana ni kimoja, na juu yake aliketi Baba na Mwana.

> *Nikatazama hata viti vya enzi vikawekwa, na mmoja aliye mzee wa siku ameketi; mavazi yake yalikuwa meupe kama theluji, na nywele za kichwa chake kama sufu safi; kiti chake cha enzi kilikuwa miali ya moto, na gurudumu zake moto uwakao.*
> *~ Danieli 7:9*

Danieli aliona viti vya enzi vikiwekwa, na hapo hasemi Mungu alivikalia vyote au kwamba vyote vilikuwa vya kwake kukalia. Cha Mungu ni kimoja na kinaonekana kuwa tofauti na viti vingine vya vya enzi. Yeye ameketi kwenye kiti kimoja na si viti vingi. Hivyo vingine wamekalia wazee ishirini na nne na wale watakaokombolewa. Ushahidi wa nabii Ellen, unafafanua zaidi kuwa kiti alichokalia Baba ndicho alichokalia Mwana. Hakuna andiko linaloonyesha kuna Viti vya Utatu (yaani wingi wa viti vya Mungu mmoja), bali mtu anaweza kuwa sahihi kusema kuna kiti cha Utatu (Utatu kwa Maana ya Mungu Mmoja mwenye nafsi tatu).

@prModa